

Chanjo za UVIKO -19 hapa Nova Scotia

miezi 6 - miaka 4 na miaka 5 - miaka 11

Umri wa miezi 6 - miaka 4

Mfululizo wa Msingi tu Pfizer ya mtoto mchanga au Moderna ya mtoto mchanga

Vipindi vilivyopendekezwa:

Moderna ya mtoto mchanga mfululizo wa msingi wa dozi 2

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 8** (siku 56)

Pfizer ya mtoto mchanga - mfululizo wa msingi wa dozi 3

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 8** (siku 56)
- ✓ Dozi 2 hadi 3 - **Wiki 8** (siku 56)



Watoto wenye umri wa miezi 6 - miaka 4 ambao **wana kinga ya mwili dhaifu kiasi au sana** watahitaji dozi ya ziada ili kukamilisha safu yao ya msingi. **Moderna ya mtoto mchanga inashauriwa.**

Moderna ya mtoto mchanga - mfululizo wa msingi wa dozi 3

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 4** (siku 28)
- ✓ Dozi 2 hadi 3 - **Wiki 8** (siku 56)

Pfizer ya mtoto mchanga - mfululizo wa msingi wa dozi 4

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 4** (siku 28)
- ✓ Dozi 2 hadi 3 - **Wiki 4** (siku 28)
- ✓ Dozi 3 hadi 4 - **Wiki 8** (siku 56)

- » Kwa kuwa idadi ya dozi za mfululizo za msingi zinatofautiana kati ya Pfizer ya mtoto mchanga na Moderna ya mtoto mchanga, watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 4 wanapaswa **kukamilisha safu yao ya msingi na aina hiyo hiyo ya chanjo.**
- » **Dozi za nyongeza** kwa sasa hazipendekezwi kwa Watoto walio katika safu hii ya umri.
- » **Baada ya kupona UVIKO-19**, watoto katika umri huu wanapaswa kusubiri **Wiki 8** kupata mfululizo wa dozi za msingi.
- » Chanjo za UVIKO-19 zinaweza **kutolewa Pamoja na chanjo nyingine.**

Umri wa miaka 5 - 11

Mfululizo wa Msingi - Pfizer (asili) Nyongeza - Pfizer Bivalent

Vipindi vilivyopendekezwa:

Kati ya dozi za mfululizo za msingi

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 8** (siku 56)

Kati ya mfululizo wa msingi na nyongeza

- ✓ **Miezi 6** (siku 168)



- » Baada ya kupona UVIKO-19, Watoto wenye umri wa miaka 5-11 wanapaswa kusubiri **wiki 8** ili kupata mfululizo wa msingi. Ikiwa wamekamaliza mfululizo wao wa msingi, wanapaswa kusubiri **miezi 6** ili kupata dozi zao za nyongeza.
- » Chanjo za UVIKO-19 zinaweza **kutolewa Pamoja na chanjo nyingine.**

Watoto wenye umri wa miaka 5-11 ambao

wana kinga dhaifu ya mwili kiasi au sana watahitaji dozi ya tatu ya chanjo ili kukamilisha mfululizo wao wa msingi.

Watoto hawa wanastahili kupata chanjo ya Moderna (asili) kama mbadala wa Pfizer.



Vipindi vya chanjo za mfululizo za msingi

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 4** (siku 28)
- ✓ Dozi 2 hadi 3 - **Wiki 8** (siku 56)

Mfululizo wa msingi mpaka muda wa nyongeza

- ✓ **Miezi 6** (siku 168)